

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

Simu ya Upopo: "KILIMO" Dodoma
Simu: +255 (026) 2321407
Nukushi: +255 (026) 2320037
Barua Pepe: ps@kilimo.go.tz
Tovuti: www.kilimo.go.tz



Idara ya Utawala,
Mji wa Serikali - Mtumba,
S.L.P. 2182,
DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

SERIKALI YAPANGA KURASIMISHA BIASHARA YA MAZAO YA KILIMO NCHINI

Dodoma, 14 Julai 2023

Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe (Mb) amefanya kikao cha pamoja na wafanyabiashara na wadau wanaouza mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi kujadili mwenendo wa usafirishaji wa mazao, jitihada za Serikali katika kuondoa vikwazo vya biashara na urasimishaji wa biashara ya mazao ya kilimo.

Waziri Bashe ameeleza kuwa takwimu zinaonesha mchango wa kilimo katika uchumi ni asilimia 26.1 ambapo mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi yameongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 994.5 mwaka 2021 hadi Dola za Marekani bilioni 1.38 kufikia Aprili 2023.

Serikali imepanga kurasimisha biashara ya mazao ya kilimo ambapo malengo mahususi ya urasimishaji huo ni kuongeza thamani ya mazao ya kilimo ili kumlinda mkulima na mfanyabiashara wa ndani dhidi ya usumbufu na utapeli unaotokea katika biashara ya mazao ya kilimo.

Aidha, Mhe. Bashe amesema kuwa Tanzania ina hali nzuri ya chakula kutokana na mavuno yaliyopatikana na kupelekeea utoshelevu wa chakula kwa asilimia 114 . Vile vile, aliwakumbusha kauli ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umuhimu wa nchi kulinda akiba ya chakula na kuwahasa wakulima kuuza ziada ya chakula popote pale duniani kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Serikali.

Mhe. Bashe amesema kuwa Serikali inaweza NFRA kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo mwaka 2030 ikiwa sehemu ya kuimarisha usalama wa chakula na lishe. Hatua nyingine ni kuongezea Wakala wa Taifa wa Uhifadhi wa Chakula (National Food Reserve Agency) uwezo wa kununua mazao ya wakulima ili kuongeza hifadhi hadi kufikia tani 500,000 na kwa msimu huu Mhe. Bashe ameagiza Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kununua mahindi kwa shilingi 1,000 kwa kilo kwa mkulima yejote anayetaka kuwauzia NFRA ofisi za Dodoma.

Kuhusu jitihada za kurahisisha usajili wa ghala za Sekta ya Umma, Sekta Binafsi na Vyama vya Ushirika, Serikali imebuni mfumo wa kidijitali unaoitwa *Crop Stock Dynamics System*. Vile vile, Mhe. Bashe amewaaahidi wafanyabiashara kuwa ataimarisha mfumo wa kidigitali wa upatikanaji wa vibali kwa njia ya mtandao ili wafanyabiashara wapate vibali kwa urahisi.

Waziri Bashe ameongeza kuwa Tanzania imekuwa katika maandalizi ya kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mifumo ya Chakula Afrika - 2023 (*Africa's Food Systems Forum*), ambao ni sehemu ya hatua za kuimarisha usalama wa chakula. Mkutano huo umepangwa kufanyaika tarehe 5 hadi 8 Septemba 2023 na utahusisha wadau mbalimbali wa kilimo na biashara kutoka ndani ya nchi, wadau kutoka Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Imetolewa na:

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini